



**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Tuesday 21 May 2002 (afternoon)

Mardi 21 mai 2002 (après-midi)

Martes 21 de mayo de 2002 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.

*Kifafanue kimoja kati ya vifungu vifwatavyo:*

**1. (a)**

	Ni ujinga wa akili Tofauti za wawili Punda kwa yake akili Punda kumwiga ng'ombe	punda kumuiga ng'ombe kama shubiri na embe hajazaliwa na pembe ni ujinga wa akili
5	Pamoja na mawakili Kwani tokea awali Wameumbwa mbalimbali Punda kumwiga ng'ombe	punda haachwi atambe hana nundu kama ng'ombe wawili hawa viumbe ni ujinga wa akili
10	Kujipa nyingi akili Kubadili wake mwili Alivyomu'mba Jalali Punda kumwiga ng'ombe	wacha tabu zimkumbe ili apate 'jipambe hageuki hata chembe ni ujinga wa akili
15	Amenyimwa na Jalali Kwa vipini na vipuli Mapozi na staili Punda kumwiga ng'ombe	'ye huyo nundu na pembe punda hampati ng'ombe hafikiki katu ng'ombe ni ujinga wa akili

Kutoka *Jua* na Mohamed Ahmed Saleh, 1997

## 1. (b)

Kutompenda Bwana Raza pamoja na utumishi wa kutwa dukani pale kulimfanya Yasmin ayachukie maisha ya unyumba na mumewe. Alitamani kufa kuliko kujitolea mwili wake kwa bwana yule. Inapofika usiku yeye huwa amejichokea na hulala mara tu baada ya kukiweka kichwa chake juu ya mto.

5 Hata baada ya kulala, Yasmin alikuwa haipati ile raha ya usingizi kwani mara kwa mara alikuwa akishtuliwa na sauti nene ya kukwaruza ya mumewe ikimwita kutoka ukumbini kumwuliza swala hili na lile.

“Yasmin!” Leo Bi. Mashavu alileta vitumbua vingapi?” Bwana Raza aliuliza, ameshughulika anafanya hesabu ya biashara ya siku ile. Yasmin huwa hajali maswali hayo na 10 huendelea na usingizi bukheri. Anapokuwa hapo Bwana Raza hushughulika kweli hataki mzaha hata kidogo na mara kwa mara Yasmin humsikia akikasirika na kugombana peke yake. Inapokuwa hivyo huwa ameshapata hasara ya kitu fulani. Malalamiko ya kupata hasara yalikuwa hayamwishi na hata siku moja hutamsikia akisema amepata faida. Hiyo ilikuwa siri aliyojua yeye mwenywewe tu.

15 Anapokuwa katika kazi hiyo ya kufanya hesabu Bwana Raza huvuta biri moja baada ya moja na moshi wa biri hizo huanikiza harufu yake mbaya nyumba nzima. Baada ya kumaliza hesabu zake Bwana Raza hufululiza moja kwa moja mpaka kitandani ambapo humkuta Yasmin amelala fo fo fo.

20 Chumba cha Bwana Raza kilikuwa kimejaa makorokcho. Mifuko ya unga, mikungu ya ndizi, maboksi ya majani ya chai na makopo ya maziwa. Kuta za chumba hicho zilikuwa zimepambwa na picha mbili tu, moja ni picha ya maandishi yaliyoandikwa kwa nakshi kwa Kiarabu majina ya Fatma, Ali, Hassan na Hussein. Picha ya pili ni ya farasi aliyebeba mkono ulioonyesha vidole vyote vitano. Mlikuwa na kiti kizuri cha msaji kilichochongwa kwa nakshi pembeni na miguuni. Bwana Raza alikinunua kiti hicho Darajani kwenye mnada. 25 Kwenye pembe nyengine ya chumba hicho mlikuwa na kiti cha marimba na juu yake palikuwa na rafu iliyogongomelewa kwa misumari ukutani. Kwenye rafu hiyo palitundikwa maguo machafu na kwenye kijiti cha mwisho cha rafu hiyo ilining'inia tasbihi ndogo.

Chumba hicho hakikuonyesha kwamba ni pahala pa mtu kupumzika. Palikuwa ni pahala pa kupitisha usiku tu, kuche, asubuhi ifike, biashara iendelee kama kawaida. 30 Anapoingia chumbani humo baada ya kumaliza shughuli zake Bwana Raza huwa hana mazungumzo tena. Ni kuvua nguo na kujitupa kitandani. Hapo hujigaragaza na kugeuka ubavu huu na huu. Mara hulala kifudifudi au mara hunyanyuka ghafla na kuwashaa taa akitafuta biri na kiberiti. Akishavipata tu vitu hivyo huwashaa biri yake na kuivuta nusu na kiasi cha kukifukiza chumba kwa moshi wa biri na halafu hujilaza tena kitandani. Hapo tena 35 humgeukia Yasmin na kuanza kumpapasa na kumtomatomasa akimwita na kumwuliza, “Yasmin ushalala?” Yasmin huwa kalala kweli, yupo mbali katika ndoto zake za kitoto. Bwana Raza humgeuza huku na huku na kumpapasapasa na mara moja moja Yasmin huzindukana na kulala tena hapohapo.

Kutoka *Vuta n'Kuvute*, na Shafi Adam Shafi, 1999